**PRIMARY EDUCATION SERVICES NETWORKING ORGANIZATION (PESNO)**

**SIMU: 0713- 526533**

**0767- 526533**

# MTIHANI WA PILI WA UTAMILIFU KWA DARASA LA SABA

# SOMO: KISWAHILI [03]

**TAREHE 03/05/2021** **MUDA: SAA 1:40**

**NAMBA YA MTAHINIWA:** ____________________________________________

**JINA LA SHULE:** ____________________________________________

**WILAYA**: __________________ **MKOA:** ___________________

## MAELEKEZO:

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya majibu
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. chagua jibu sahihi kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia (OMR)kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya (OMR)
5. Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi

**6**. Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa

## SEHEMU A: CHAGUA JIBU SAHIHI

## UJUZI WA KUSIKILIZA, SARUFI NA LUGHA YA FASIHI

1. Kijiji cha Mwendokasi kipo karibu na hifadhi gani?
   A. Mlomazi B. Mkomazi C. Mikumi D. Saa nane E. Ngorongoro
2. Busara na bibi yake walikwenda wapi siku ya Jumamosi?
   A. Porini B. Kwenye hifadhi C. Shambani D. Njiani E. Kijijini
3. Nani alikuwa wa kwanza kuwaona tembo?
   A. Bibi B. Busara C. Ng’ombe D. Wote E. Shaibu
4. Kisawe cha tembo kama ilivyotajwa kwenye habari uliyosikiliza ni:
   A. Shibli B. Nyati C. Ndovu D. Ngamia E. Kangaroo
5. Maneno “amepigwa na butwaa” kama yalivyotumika kwenye kifungu cha habari yana maana gani?
   A. Huzunika B. Shangaa C. Pigwa na mchecheto D. Fukuza ndovu E. Takasa
6. Vyakula vilivyopakuliwa jana vimeliwa leo asubuhi. Hii ni aina ipi ya sentensi?
   A. Sahili B. Changamano C. Shurutia D. Ambatano E. Huru
7. Chakula chaliwa sebuleni na wanafunzi wote. Tungo hii ipo kwenye hali gani?
   A. Timilifu B. Endelevu C. Isiyodhihirika D. Ukanushi E. Ya kawaida
8. Mzee Gabriel angelima kwa bidii _______________ mazao ya kutosha:
   A. Angelivuna B. Angelilivuna C. Angalivuna D. Angevuna E. Atavuna
9. Maneno “kope, nyasi, nyusi na nywele” kwa paoja yapo katika ngeli ya:
   A. I—ZI B. KI—VI C. U—ZI D. KU E. U—YA
10. Wanafunzi waliofaulu lugha ……..Hii ni aina ipi ya tungo?
   A. Sahili B. Tegemezi C. Huru D. Changamano E. Ambatano
11. Mzee Mfinanga ni Hodari wa kudunduliza. Neno kudunduliza maana yake ni:
   A. Kudodosa B. Kukusanya miganda miganda C. Kuweka kidogo kidogo
   D. Pewa riba ndogo ndogo E. Chembe na chembe mkate huwa
12. Mwenyewe hawezi kuwapa nasaha zozote. Neno mwenyewe ni aina ipi ya kiwakilishi?
   A. Kiwakilishi cha pekee C. Kiwakilishi cha nafsi
   B. Kiwakilishi cha idadi D. Kiwakilishi cha sifa E. Kiwakilishi cha a-unganifu
13. Mofimu ya kutendwa kwenye kitenzi “Bembelezwa” ni:
   A. —Lez— B. Bembelez— C. –W D. —W— E. —Wa
14. Andika umoja wa sentensi ifuatayo kwa usahihi “Nyusi zangu zimenyofoka”
   A. Nyusi wangu umenyofoka C. Kanyusi kangu kamenyofoka
   B. Unyusi wangu umenyofoka D. Minyusi yetu imenyofoka E. Tunyusi twetu tumenyofoka
15. “Mama atakuwa analima mpunga kesho” Dada alisema. Ipi ni kauli taarifa ya kauli hii?
   A. Dada alisema kwamba mama atakuwa analima mpunga kesho
   B. Mama atakuwa analima mpunga kesho mama alisema
   C. Dada alisema mama angekuwa analima mpunga siku iliyofuata
   D. Dada alisema kwamba mama angekuwa analima mpunga kesho
   E. Mama analima mpunga

16. Kauli ipi si sahihi kuhusu kadi ya mwaliko kati ya hizi?
   A. Huwa na jina la mwandishi   C. Jina la mwandikiwa huweza kuanza kwa cheo
   B. Huwa na jina la mwandikiwa   D. Huwa na sehemu au mahali pa tukio   E. Saini ya mwandishi
17. Mtu anapostaafu hupewa ______________ ili aweze kujikimu katika maisha yake:
   A. Penseli   B. Posho   C. Kiinua mgongo   D. Mshahara   E. Hongo
18. Jambo, tukio au hali inayosababisha mtu kuwa na huzuni mfano ajali, kufiwa, kuibiwa n.k huitwa:
   A. Kifo   B. Huzuni   C. Rambirambi   D. Msiba   E. Jambazi
19. Asili au chimbuko la maneno katika kamusi linaloelezewa na kuoneshwa kwenye kitomeo huitwa:
   A. Kidahizo   B. Kitomeo   C. Matini ya kamusi   D. Mwanzo wa kamusi   E. Etimolojia
20. Neno “Peremende lina aina ngapi za vokali?
   A. 4   B. 5   C. 6   D. 8   E. 1
21. Methali ipi inashabihiana kimaana na methali “Ng’ombe haelemewi na nunduye?”
   A. Haba na haba hujaza kibaba   C. Mlinzi wa kisima hafi kiwi
   B. Boga baya lipo shambani mwako   D. Huku pi n akule pi   E. Halahala mti na macho
22. “Athari ya kidole ___________”. Kamilisha methali hii:
   A. Kucha kuchomoka   C. Hasara ya mwili
   B. Usaha hutumbuka   D. Ukamtia mkono kinywani   E. Mkono hukatwa
23. Tegua kitendawili “Watumwa Weusi wananing’inia mtini”
   A. Waafrika   B. Bilinganya   C. Fenesi   D. Mkaa   E. Korosho
24. Nahau ipi ina maana ya kupatwa na hasira au kughadhabika kutokana na jambo fulani?
   A. Noa ulimi   B. Kata maji   C. Panda mori   D. Pata moto   E. Vimba kichwa
25. Si jambo jema kumtendea ubaya mtu aliyekufanyia badala yake tuwatendee mazuri na kuwakirimia. Methali ipi inaendana na maelezo haya?
   A. Penche penche ni penche na penche   C. Akufanyiaye ubaya mlipe wema
   B. Chuma kukatika si kosa la mhunzi   D. Njia mbili zilimshinda fisi   E. Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha
26. “Ukiona njigi utadhani njege na ukiona njege utadhani njigi” tegua kitendawili hiki:
   A. Maziwa na tui la nazi   C. Mzungu na Mchina
   B. Mwezi na jua   D. Popo na ndege   E. Nywele na manyoya
27. “Daima damu yangu hunyonywa na kuuzwa lakini bado nipo imara” Tegua kitendawili hiki:
   A. Mbu   B. Binadamu   C. Maji   D. Utomvu wa mpira   E. Upepo
28. Nahau “ng’ata sikio” na “uma sikio kwa Pamoja zina maana gani?
   A. Kuonywa   B. Kuapishwa   C. Kunong’onezwa   D. Kunyofolewa sikio   E. Kupigwa
29. Mwalimu ameletewa zawadi nzuri. Sentencsi hii ipo katika kauli gani
   A. Kutendwa   B. Kutendewa   C. Kutendeka   D. kutendeana   E. Kutendesha
30. Kauli ipi si sahihi kuhusu methali?
   A. Methali huwa na pande mbili   C. Methali huwa na maana fiche
   B. Methali huwa na funzo   D. Methali hupotosha jamii   E. Methali si kitendawili
31. Tabia ya kuandika barua kwa kutumia misimbo ilikuwa imekita mizizi miongoni mwa wanafunzi. Usemi kita mizizi una maana gani?
   A. Imarika   B. Chimbika   C. Bomoa   D. Zembea   E. Pendwa

32. Sikuchukua kalamu_______ kutoka kwake. Neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi

A. Yeyote B. lolote C. yoyote D. wowote E. chochote

33. Mtu mwenye ulemavu wa ngozi hujulikana kama

A. Kilema B. chotara C. shombe D. zeruzeru E. hafukasti

34. Wingi wa neno saa ni upi?

A. Misaa B. muda C. Masaa D. lisaa E. saa

35. Mtu anayetunza vitu katika ghala au bohari huitwaje?

A. Mkufunzi B. mhuzini C. baharia D. mwana E. boharia

## SEHEMU B: UTUNGAJI

**Umepewa sentensi ambazo hazina mpangilio rasmi zipange vizuri ili ziweze kusomeka vizuri kwa kutumia herufi A, B, C, D, na E**

36. Mhimili mmojawapo aliousikia ni bunge
37. Siku moja akiwa shuleni, alimwomba mwalimu wake amweleze zaidi kuhusu bunge
38. Kapesa anasoma darasa la saba katika shule ya msingi Kikombo
39. Mwalimu alikubali na kumwahidi Kapesa kuwa atafanya hivyo darasani
40. Aliwahi kusikia kuhusu mihili ya dola

## SEHEMU C: USHAIRI

**Soma shairi lifuatalo na ujibu maswali yanayofuata**

Nimefika bandarini, sitaki tena safari,
Bahari siitamani, si kwa nguvu si hiyari,
Usafiri wa majini, kwangu mimi si mzuri.

Dhoruba ilinipata, katikati ya bahari
Radi nazo zilidata, mvua nazo zilkajiri
Na tufani zikafata, koma tupo hatarini

Utwesi ukenda kombo, zikaingia kikiri
Mrama kikenda chombo, tukawaza furifuri
Mawimbi kupiga kumbo, hamkani siyo shwari

**MASWALI**

41. Shairi hili lina beti ngapi?
42. Vina vya mwisho kwenye beti zote ni vipi?
43. Shairi hili limetumia muundo wa
44. Andika kituo cha shairi hili
45. Mwandishi wa shairi hili ametumia aina gani ya kituo?